# Uibukaji wa U-Nigeria katika Tasnia ya Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania: Masuala Muhimu ya Kuzingatia

**Gervas A. Kasiga**
*Chuo Kikuu cha Dodoma*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2022-12-12*
*Rekebishwa: 2023-01-01*
*Kubalika: 2023-04-28*
*Chapishwa: 2023-05-20*

***Maneno Muhimu***
Uibukaji
U-Nigeria
Tasnia
Muziki
Kizazi Kipya

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Kasiga, G. A. (2023). Uibukaji wa U-Nigeria katika Tasnia ya Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania: Masuala Muhimu ya Kuzingatia. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *1*(1), pp. 18-30.

*Copyright © 2023 The Author*
CC BY

**Ikisiri**
Imebainika kuwa tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania imetekwa na utamaduni wa nje hususani wa Kinigeria (Mrikaria, 2007; Kasiga, 2022). Athari zake zimebainika katika vipengele kadhaa vya kibunifu (Kasiga, 2021). Pia, misukumo mbalimbali inayowasukuma wasanii kutumia U-Nigeria imebainishwa (Kasiga, 2022). Kimsingi, hali hii inatishia utambulisho wa Kitanzania katika sanaa. Hivyo, makala hii imetoa mapendekezo ya kiuboreshaji dhidi ya U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Mapendekezo yaliyotolewa yamehusisha: kufanyika uwekezaji wa muziki wa asili wa Kitanzania, kufanyika kwa usimamizi maalumu katika vyombo vya habari, kuwepo kwa sheria na kanuni za kulinda uasili wa muziki wa kizazi kipya, na uanzishwaji wa semina, warsha pamoja na madarasa maalumu kwa wasanii. Isitoshe, makala imependekeza kuwepo kwa agenda mahususi ya kitaifa kujenga uzalendo, kumakinikia mitindo ya sanaa za Kitanzania katika utengenezaji wa muziki, kuharakisha upatikanaji wa vazi la taifa, kuanzishwa kwa vipindi vya uchambuzi wa nyimbo, na wasanii kushawishiwa kutumia mandhari ya Kitanzania katika video zao. Zaidi, imependekezwa kuanzishwa kwa matamasha na tuzo za muziki, asasi za elimu kutengeneza mitaala ya biashara, lugha ya Kiswahili, na utamaduni wa Kitanzania, na kuwe na muumano kati ya biashara, utamaduni na teknolojia.

## Utangulizi

U-Nigeria ni hali ya filamu kuwa na vionjo vya kitamaduni vinavyotokana na jamii tatu kubwa za Kinigeria – yaani jamii za Waigbo, Wayoruba na Wahausa (Haynes & Onookome; Kasiga, 2013). Vionjo vya Kinigeria aghalabu hujipambanua kupitia mavazi, mandhari, vifaa vya kijukwaa, ala na midundo ya kimuziki na matumizi ya lugha (Kasiga, 2022). Makala hii imesukumwa na tafiti

zilizotangulia kuhusu U-Nigeria katika Fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania (Kasiga, 2013; Kasiga, 2018; Kasiga & Luhwago, 2020; Kasiga, 2021; Kasiga, 2022). Tafiti hizo zilibaini kuwa kuna athari kubwa ya matumizi ya U-Nigeria ndani ya Fasihi ya Kiswahili ya kisasa nchini Tanzania. Katika tafiti hizo ulibainishwa mdhihiriko wa U-Nigeria kupitia Filamu Ndefu za Kiswahili na Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya wa Kiswahili (Kasiga, 2013; Kasiga, 2019). Licha ya kubainishwa kwa mdhihiriko huo, bado U-Nigeria ulibainika kuwa athari kubwa katika filamu na video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili (Mrikaria 2007; Samwel, 2015; Kasiga, 2018; Kasiga, 2021). Katika tafiti hizo U-Nigeria ulibainishwa kwa mizani ya tija na madhara yake kwa Watanzania.

Hali kadhalika, sababu za kutumiwa U-Nigeria katika sanaa za Kiswahili nazo zilibainishwa (Kasiga, 2013; Kasiga, 2022). Hata hivyo, licha ya mchango mkubwa uliotolewa na tafiti hizo bado kuna sehemu muhimu haikuzamiwa kwa kina. Mwanya huo ni utoaji wa mapendekezo ya kiuboreshaji dhidi ya madhara yanayotokana na U-Nigeria. Hivyo basi, katika makala hii tuliona ni muhimu tujikite kutoa mapendekezo kuhusu namna ya kuondokana na U-Nigeria katika Fasihi ya Kiswahili. Ni imani yetu kuwa mapendekezo yaliyotolewa yataufanya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wa Kitanzania uweze kuiakisi jamii yake.

**Nadharia ya Upembetatu wa Ki-Aristotle**

Mapendekezo yaliyoibuliwa na makala hii yalisukumwa na Nadharia ya Upembetatu wa Ki-Aristotle. Nadharia hii inaitazama fasihi kama zao la jamii. Hivyo, sanaa iliyozamiwa ilitarajiwa itokane na jamii husika. Mathalani, muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania ulitarajiwa utokane na mifumo ya kijamii na utamaduni wa jamii ya Kitanzania. Nadharia hii, kwa kiasi kikubwa, inamzungukia Aristotle. Aristotle alianzisha uchambuzi wa kisayansi wa kifasihi na nadharia zake zimeathiri mikabala kadhaa ya karne ya 20. Uhakiki wake ulihusisha fani za ushairi na tamthiliya na kuibua nadharia jumuishi inayoeleza kwamba ushairi na tamthiliya ni stadi kama zilivyo aina nyingine za sanaa (Mulokizi, 2017). Pia, nadharia yake inaeleza kuwa mwigo katika sanaa ni jambo la msingi na halipaswi kubezwa. Aliamini kuwa mwigo katika uumbaji wa sanaa huambatana na ubunifu wenye kubeba ukweli wa kijamii. Alitazamia simulizi ya hadithi iwe na mfuatano wa kimantiki wa matukio kuanzia chini mpaka kwenye kilele. Anaeleza kuwa katika kufanya tathimini, kuna ulazima wa kuzingatia msuko (ploti), wahusika, mawazo, ufundi wa kutumia lugha (ulonzi), muziki, na shani. Vilevile, katika hadithi ni vema kuwe na wazo moja kuu unganifu. Kimsingi, msisitizo mkubwa wa Nadharia ya Upembetatu wa Ki-Aristotle unabainisha kuwa nguvu ya usanii hutokana na uzoefu wa msanii katika mazingira yake na kiwango cha ufahamu wake. Umuhimu wa kazi ya sanaa kwa jamii unatokana na jinsi msanii anavyohusisha usanifu wake na matukio muhimu yanayomzunguka. Hakuna shaka kwamba kuna mapatano makubwa kati ya msanii, kazi ya sanaa na hadhira yake. Mapatano haya ya kijamii licha ya kuisogeza sanaa mahali pake stahiki, yaani kwa wanajamii wake, pia huleta ukamilifu wa mawasiliano baina ya sanaa na wanajamii wake. Aidha, ikifanyika hivyo huongeza thamani ya sanaa husika kwa jamii yake na kwa jamii nyingine.

Uchambuzi wa Ki-Aristotle hufanyika kupitia vijenzi vya kazi ya kisanaa ambavyo mchambuzi huvichagua kuendana na mahitaji ya utafiti wake. Msokile (1993) anasema kuwa kupitia Upembetatu wa Ki-Aristotle, kuna mambo manne muhimu ya kuyaangazia: kwanza, ni kazi yenyewe inayochambuliwa ambayo ni zao la mawazo ya binadamu; na suala la pili muhimu kuangalia ni mwanasanaa. Suala la tatu muhimu ni mazingira ambayo kazi ya sanaa imeandikiwa. Mazingira

hutazamwa kwa sababu athari mbalimbali za kifani na kimaudhui zinatokana na mazingira hayo. Mazingira ya mwandishi/msanii hujumuisha watu na mawazo yao. Na jambo la mwisho muhimu katika kuchambua kazi ya sanaa ni hadhira ambayo imekusudiwa na kazi hiyo. Hadhira hii ni wale watu wanaosikiliza, watazamaji na wasomaji ambao kwao kazi ya kisanaa imekusudiwa.
Jengo na Wenzake (1982) wanakazia umuhimu wa nadharia hii kwa kumakinia kuwa, ikiwa tunakubali kwamba sanaa ni fani maarufu ya utamaduni wa binadamu, basi ni dhahiri kwamba mazingira ya binadamu yanatofautiana, na ni wazi kwamba hata falsafa ya fani mbalimbali za utamaduni wa binadamu zinatofautiana. Hivyo, ni makosa kwa mtaalamu kuukubali bila kusita uchambuzi wa kifalsafa usio na misingi ya mazingira yake ya kiutamaduni. Wakati huo katika kuzidi kuifafanua nadharia hii na matumizi yake, Devereux (2010) anasema kuwa uundwaji wa Upembetatu wa Ki-Aristotle katika uhakiki huongeza uwezo wa taaluma ya uchanganuzi wa filamu, hususani katika kutazama jinsi filamu zinavyoathiri watazamaji wake kiujumi baada ya kutazamwa.

Mwelekeo mkubwa wa Nadharia ya Upembetatu wa Ki-Aristotle umejikita zaidi katika kuiunganisha sanaa na hisia. Kwa hali hiyo, maunzi/misingi minne inayotokana na muunganiko wa kazi ya kisanaa, mtunzi na mtumiaji wa sanaa ndiyo ilitumika katika kusaidia uchambuzi ulioleta matokeo ya makala hii. Maunzi hayo manne ambayo yamesukuma mapendekezo yetu ya kiuboreshaji ya tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania ni:

a) Viunzi kwa mantiki ya lugha ndani ya video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya;
b) Fani na umbo zima la kazi ya kisanaa;
c) Kielenzo/Kisababishi kilichomsukuma msanii kuunda kazi husika ya kisanaa;
d) Hitimisho au/na matokeo ya kazi husika ya kisanaa pamoja na athari inayoibua.

Katika kufanya uchambuzi wa data zetu, misingi yote minne ilitumika kwa mantiki ya kuangazia namna tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili inavyoakisi jamii husika iliyolengwa na inayopelekewa kazi husika ya kisanaa. Tulichobaini ni kuwa jamii ya Kitanzania haikuakisiwa ipasavyo katika tasnia hiyo. Zaidi, matokeo ya utafiti wa makala yalidhihirisha uakisi mkubwa wa utamaduni wa Ki-Nigeria katika tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kitanzania. Hivyo, ni sawa na kusema kuwa nguvu ya usanii wa wasanii haikujinasibu kutokana uzoefu wa msanii katika mazingira yake na kiwango cha ufahamu wake. Wakati inapaswa umuhimu wa kazi ya sanaa kwa jamii itokane na jinsi msanii anavyohusisha usanifu wake na matukio muhimu yanayomzunguka. Hakuna shaka kwamba kuna mapatano makubwa kati ya msanii, kazi ya sanaa na hadhira yake. Mapatano haya ya kijamii, endapo yangeonekana katika tasnia ya muziki wa kizazi kipya, yangeisogeza tasnia mahali pake stahiki, yaani kwa wanajamii wake. Kudhihirika kwa jambo hilo kungeleta ukamilifu wa mawasiliano baina ya sanaa na wanajamii wake. Hivyo basi, katika sehemu inayofuata katika makala hii mapendekezo ya kiuboreshaji wa tasnia yametolewa ili kusaidia tasnia ya muziki wa kizazi kipya kuwa zao la jamii ya Kitanzania.

**Mapendekezo ya Kiuboreshaji**
Kingengele hiki kinatoa mapendekeo ya kiuboreshaji dhidi ya U-Nigeria katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Kasiga (2022) katika tathimini aliyofanya kuhusu faida na hasara za U-Nigeria katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, amebainisha kuwa hasara ni kubwa kuliko faida. Hii inatokana na ukweli kwamba, licha ya U-Nigeria kuleta kipato kwa

wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili, madhara yake ni makubwa katika utamaduni wa Kitanzania. Jambo jingine ni kuwa, faida ya kisoko na kibiashara inayopatikana kupitia idadi wa wasanii tulionao, bado si ya kuridhisha. Imebainika kuwa tasnia ya muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania imeshindwa kukuza vipaji vingi na kuvikuza kufikia viwango vya kimataifa. Ni wasanii wachache tu kutoka vikundi vya muziki/rekodi za muziki vya/za Wasafi Classic, Konde Gang na Kings Music ndio waonashika chati za muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania. Kupitia makala, ilibainika kuwa makundi hayo yamebeba wasanii wachache tu (Kasiga, 2022). Mathalani, rekodi ya muziki wa Wasafi Classic ina wasanii sita tu ambao ni Nassib Abdul (Diamond Platinumz), Raymond Shabani (Rayvanny), Mbwana Yusuph Kilungi (Mbosso), Zuhura Othman Soud (Zuchu), Abdul Juma Idd (Lavalava), na Mwanahawa Abdul Juma (Queen Darlin). Rekodi Konde Gang Music ina wasanii wawili ambao ni Rajab Abdulkahali Ibrahim (Harmonize) na Ibrahim Abdallah Nampunga (Ibraah). Huku rekodi ya muziki ya Kings Music ikiwa na wasanii wanne tu ambao ni Ali Kiba, Abdul Kiba, Karim Zuber Rashid (K2ga), na Thomas Gration Bishanga (Tommy Flavour). Hivyo, kupitia makala hii, imethibika kuwa kupitia U-Nigeria, mafanikio ya kitasnia si ya kiwango cha kuridhisha. Hii ni kwa sababu, wasanii wachache tu hufaidika na utumiaji wa U-Nigeria katika video za nyimbo zao. Hii limebainika kupitia uchambuzi wa mauzo ya wasanii kupitia mitandao ya kijamii mathalani mtandao wa YouTube.

Kwa hali hiyo, wasanii wengi wanaochipukia, licha ya kuvutika kufanya muziki wao kwa kutumia vionjo vya ki-Nigeria, bado hawajaweza kuvuka viwango vya kimataifa. Kupitia utafiti wa makala hii, ilibainika kuwa licha ya wasanii kushindwa kufikia viwango vya kimataifa, papo hapo wanakuwa wamepoteza uwezo wao wa kunyanyua muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Hivyo, kwa kiasi kikubwa, U-Tanzania[1] uliopotezwa katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili unazidi kupunguza mambo muhimu ya kimaadili katika jamii na kitamaduni. Mambo hayo yangewekewa mkazo, huenda yangeweza kufungua fursa nyingine za kibiashara kwa vijana wengi kuweza kuuza utamaduni wa Kitanzania kupitia tasnia nzima ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Hivyo, katika kuangalia namna ya kuukuza muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania na kuufanya uwe endelevu kibiashara, huku ukinyanyua utamaduni wa Kitanzania na maisha yake ya kijamii, utafiti umeibua mapendekezo yafuatavyo:

**Kufanyika Uwekezaji wa Muziki wa Asili wa Kitanzania**

Katika kutatua changamoto hii ya asilimia kubwa ya U-Nigeria uliopo katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, ni muhimu kufanywa uwekezaji mkubwa katika muziki wa asili wa Tanzania. Hili linaweza kufanyika kupitia tafiti za kina zitakazoendeshwa katika jamii zinazopatikana nchini Tanzania. Tanzania imebarikiwa kuwa na jamii zenye vipengele vingi na tofauti vya utamaduni. Hivyo, tafiti zinatakiwa kufanyika kwa kina na mapana ili kuweza kutengeneza ladha ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Isitoshe, ni muhimu kuzikuza kwa kuziweka kiteknolojia nyimbo, ngoma, na mitindo mingine ya kiasili. Kufanyika kwa tafiti hizi kunaweza kunyanyua mitindo na mipigo mbalimbali ya muziki wa kizazi kipya itakayotoka

[1] Mathalani katika mavazi, ala na midundo inatoa taswira za kifasihi, mitindo ya uchezaji, mandhari za zanye motifu za Ki-Nigeria, utumiwaji wa vifaa vya kijukwaa, na matumizi ya lugha.

katika jamii za Kitanzania. Hili litaenda sambamba na uwezo wa kuchukua mitindo ya uchezaji ya jamii za Kitanzania na kuipa nafasi katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili.

Katika utekelezaji wa jambo hili, ngoma za asili, pamoja na sanaa nyingine za asili, zinatakiwa kuanza kufundishwa kutoka shule za awali na msingi. Jambo hili linaweza kuweka jiwe zuri la msingi kwa watoto ambao watathamini mila na desturi zao. Pia, endapo watakuja kuwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya katika miaka ya baadaye, itawasaidia kuboresha tasnia ya muziki kupitia asili yao. Mwanzoni, jambo hili lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa, wakati wa uongozi wa kitaifa wa Awamu ya Kwanza na ya Pili nchini Tanzania. Katika uongozi wa Awamu ya Kwanza nchini Tanzania, chini ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kulifanyika tafiti zilizofanikisha kuteuliwa kwa ngoma ya jadi ya "Sindimba" kutoka kusini mwa Tanzania ambayo ilikuwa inafundishwa na kuchezwa katika shule zote za msingi na sekondari nchini Tanzania. Vilevile, katika ukuzaji wa sanaa, kuliundwa kikundi cha sanaa cha taifa ambacho, baadaye, kutokana na kuonekana kwa umuhimu wa sanaa katika maendeleo ya kitaifa. Miaka michache baadaye, kikundi hicho kikawa sehemu ya uanzishwaji wa Chuo cha Sanaa cha Bagamoyo, hivi sasa, Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TASUBA). Licha ya kutokupewa umuhimu mkubwa kwa awamu za uongozi zilizofuatia, juhudi hizi zinatakiwa zirejeshwe na kutiliwa maanani, na kuendelezwa.

Katika kufanikisha mapendekezo haya, tunaweza kuangalia namna nchi ya Afrika Kusini ilivyofanikiwa kukuza biashara ya muziki wake wa kizazi kipya, na papo hapo ikiuza utamaduni ndani ya muziki huo. Katika nchi hii, kwa mfano, wasanii wa kundi la Mafikizolo wamejenga mazoea ya kuchukua nyimbo na vionjo vya asili kutoka utamaduni wa Kizulu na Kixhosa, na kisha kuviboresha katika studio za muziki za kisasa. Kupitia jambo hilo, utunzaji wa ladha ya asili na utamaduni wa muziki imebakia kwa namna kubwa. Kwa Tanzania, inawezekana kuuvumbua na kuutunza muziki wetu. Kuna haja ya tafiti za kina za masuala ya jadi na utamaduni kufanyika katika jamii (makabila) yote. Hivyo, makala inapendekeza ngoma kutoka jamii za Kitanzania kufanyiwa utafiti kuona namna zinavyoweza kufundishwa shuleni na vyuoni. Makala inaona kuwa kufanyika kwa jambo hilo, kutatuwezesha kupata muziki bora wa kizazi kipya kama ambavyo ilishawahi kutokea kwa Marehemu Mr. Ebbo, kundi la Mambo Jambo, Marehemu Che Mundugwao, na kundi la Tatu Nane. Wasanii wengine walikwishaonesha njia katika jambo hili ni Saida Karoli, Marehemu Dkt. Hukwe Zawose, Marehemu Mzee Moris Nyunyusa, Marehemu Mubaraka Mwinshehe, Marehemu Marijani Rajab, Marehemu Patrick Balisidya na Marehemu Moshi William. Jambo hili linahitaji mipango madhubuti na uwekezaji wa muda mrefu.

**Usimamizi Maalumu katika Vyombo vya Habari**

Makala inapendekeza kuwa katika vyombo vya habari nako kunatakiwa kuwekewe usimamizi maalumu. Matokeo ya makala yanaonesha kuwa vyombo vingi vya habari nchini Tanzania, hupiga zaidi nyimbo na video za nyimbo za muziki wa Ki-Nigeria na nyingine zenye maudhui ya nje. Upigaji huo wa maudhui ya nje licha ya kudumaza masikio ya wasikilizaji na watazamaji wa Kitanzania, pia husababisha wasanii nao kuchukua mkondo wa kubeba mahadhi ya nje katika kuunda muziki wao. Kwa hiyo, jambo la awali na muhimu la kufanyika ni kuhakikisha watangazaji wanaofanya kazi katika vituo vya redio na runinga nchini Tanzania wanapatiwa elimu maalumu yenye lengo la kuona umuhimu wa kudumisha mila, desturi na tamaduni za Kitanzania kupitia muziki wa kizazi kipya wa

Kiswahili. Jambo hili likifanyika litasaidia kukomesha na kurudisha muziki wenye maudhui ya asili ya Kitanzania.

Katika kufanikisha suala hili, makala inapendekeza kuwa vyombo vya habari vya Kitanzania vinatakiwa kupunguza kupiga muziki wenye mahadhi ya Kinigeria. Kwa kupunguza kuupiga muziki wa Kinigeria, kutaudhoofisha na hivyo kusaidia wasikilizaji na watazamaji kurudi katika muziki wa kizazi kipya wenye asili ya Tanzania. Vilevile, vyombo vinavyohusika na ukuzaji na uendelezaji wa sanaa nchini Tanzania vinatakiwa kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kutengeneza sheria na kanuni ndogondogo zitakazohakikisha zinalinda maudhui ya ndani ya muziki wa Kitanzania. Aidha, kunatakiwa kuwe na sheria zitakazotoa miongozo ya kupiga muziki wa ndani wa Tanzania kwa asilimia 75 na asilimia 25 zilizobaki ziwe kwa ajili ya muziki unaotoka nje ya Tanzania. Pia, vyombo vyetu vya habari vioneshe makusudio ya dhati ya kutoa kipaumbele kwa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wa nchini Tanzania.

**Kuwapo na Sheria na Kanuni za Kulinda Uasili wa Muziki wa Kizazi Kipya**

Makala inapendekeza kuwapo kwa sheria na kanuni ili kulinda uasili wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Pia, kuwe na miongozo itakayohakikisha wasanii wote wa muziki wa Tanzania wanasajiliwa na kufahamika. Hili liende sambamba na kuwasajili wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Jambo hili litasaidia kuirasimisha sanaa ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili, pamoja na wasanii wake. Kanuni hizi dhidi ya wasanii zihakikishe kuwa pindi msanii wa kizazi kipya atakapofanya ushirikiano wa kisanii na mwanamuziki kutoka nje ya Tanzania, basi itamlazimu asiende mbali na aina ya muziki wa kizazi kipya wa Kitanzania. Aidha, kuwe na wataalamu watakaopima asilimia ya vionjo vya muziki vitakavyotengeneza mchanganyiko katika muziki utakaofanywa baina ya msanii wa nje ya Tanzania na msanii wa ndani ya Tanzania. Jambo hili linatakiwa lichukuliwe mfano kutoka kwa wasanii wa muziki wa singeli ambao huwa hawabadiliki katika maudhui, fani na mazingira ya muziki wao, hata wanaposhirikishwa na wanamuziki wengine. Mambo hayo yakifanyika yatatia chachu katika kukuza na kuuendeleza muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Pia, taratibu maalumu zinatakiwa kuwekwa ili kuhakikisha kwamba msanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili anapoenda kuwakilisha nchi nje ya Tanzania afanye muziki utakaokuwa na nguvu ya kuitangaza Tanzania. Hili litaondoa jambo lililozoeleka kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kutokea nchini Tanzania kujikuta wakitumbuiza nje na kuchukua tuzo, ilihali muziki walioufanya umebeba maudhui na fani ya kigeni.

Vilevile, kunatakiwa mkazo mkubwa uwekwe katika kupiga muziki wa ndani (Tanzania) katika sehemu za burudani kama vile kwenye sherehe za harusi, sehemu za kupata vinywaji na nyingine za kumbi za starehe. Elimu pia inahitajika katika maeneo haya. Hii ni kwa sababu wadau wakubwa wa muziki ndio huchangia katika ukuaji au/na ubomoaji wa maadili na utamaduni wa wa Kitanzania kupitia tasnia ya muziki. Suala la kuona umuhimu wa kupiga muziki wa nyumbani katika sehemu za starehe liangaliwe kupitia mafanikio yaliyofanyika katika nchi za Nigeria na Afrika Kusini. Katika nchi hizo kumbi za starehe hupiga muziki wa ndani. Jambo hilo limefanikisha kwa kiasi kikubwa kukuza na kuuendeleza muziki wao ndani ya nchi zao, kisha kuvuka mipaka nje ya nchi hizo. Nchini Tanzania kumbi za starehe hupiga muziki kutoka nje ya Tanzania kwa asilimia kubwa kuliko muziki wa ndani. Ni imani yetu kuwa kama nyimbo za muziki wa Kitanzania zitapewa kipaumbele cha kupigwa katika sehemu hizi utaongezewa thamani yake na papo hapo kuongeza kiu kwa washabiki

wa ndani wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kuusikiliza na kupenda sanaa za ndani ya nchi yao.

**Uanzishwaji wa Semina, Warsha, na Madarasa Maalumu kwa Wasanii**

Wasanii wanatakiwa kupatiwa semina na warsha kuhusu tasnia ya muziki. Lengo kuu la semina na warsha hizi liwe katika kuwajenga kitasnia na utamaduni wa Kitanzania. Jambo hili linashauriwa liende moja kwa moja katika kuwahimiza kuimba nyimbo zitakazoepuka kuchota motifu za muziki wa nchi za nje kama ulivyo. Wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili waelekezwe na kuongozwa katika kujikita na kujifunza Fasihi Simulizi ya Kitanzania, pamoja na maonesho ya sanaa za kiasili za jamii wanazotoka. Kwa kufanya hivyo, kutawasaidia kuweza kuingiza vionjo vya kitamaduni vya muziki wa asili wanamotoka na kuuhusisha katika muziki wao wa kizazi kipya wa Kiswahili. Upanukaji wa jambo hili utakuwa na athari chanya katika muundo wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili utakaokuwa ukitengenezwa na kuingia sokoni.

Kuchukua mitazamo hii mipya kutasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kuweza kujitanua katika utajiri mkubwa wa kitamaduni wa jamii (makabila) 120 zilizopo nchini Tanzania. Pindi watakaponakili sauti, ala, mavazi na masuala mengine ya kijamii ya Kitanzania, moja kwa moja yataupa taswira mpya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wa nchini Tanzania. Kufanyika kwa jambo hilo kutasaidia kupunguza au/na kuondoa hali ya unakili wa vionjo vya Kinigeria katika muundo mzima wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania.

Katika suala la elimu, vyombo vinavyosimamia ukuzaji na uendelezaji wa sanaa na muziki nchini Tanzania vinatakiwa kusaidia kutoa elimu kwa wasanii kuhusu muziki wanaoufanya, yaani muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Elimu hii itakapotolewa itawasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kujitambua. Kujitambua huku kutaongeza ari katika kufanya muziki wa kizazi kipya ambao hautakuwa ukiachana na mila, desturi na tamaduni zake. Kwa kufanya hivyo, itawasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya kuwa na malengo mapana kuhusu muziki wao na kufahamu matokeo ya sanaa wanayofanya kijamii na kinchi. Makala inaona kuwa hili litasaidia kuondoa dhana ya msanii wa Kitanzania kujikuta licha ya kufanya muziki wa kigeni bado anakuwa amejitwisha lakabu kutoka jamii ya kigeni. Elimu itakayotolewa, vilevile, inapendekezwa ijikite katika kueleza namna uchotaji wa maudhui na fani ya kigeni katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili inavyoweza kuleta madhara kwa jamii yetu. Hii itasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kuweza kuelewa ni kwa namna gani sekta ya muziki inavyoweza kujenga, kuenzi, na kuboresha maisha na mtazamo wa kitamaduni wa jamii ya Kitanzania.

**Kuwepo na Agenda Mahususi ya Kitaifa ya Kujenga Uzalendo**

Makala imebaini kuwa, hadhira nayo imeonekana kuvuta wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kutumia ugeni. Hivyo, nayo inafaa kupatiwa elimu ya kuthamini sekta ya muziki ya ndani. Hili linaweza kufanyika kwa kuwa na vipindi vya mijadala vya kiburudani katika redio, televisheni, na mitandao ya kijamii. Vipindi na mijadala hiyo itatakiwa ijielekeze na kujikita katika mijadala yenye kutoa muelekeo thabiti wa tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Mijadala hii inatakiwa ifanyike kwa kushirikisha maoni na mitazamo ya hadhira ya muziki huu. Jambo hili likifanyika huenda litaleta nguvu kubwa katika kurudisha upenzi wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili.

Muktadha wa suala hili ni mpana. Hivyo basi, bado litahitaji ushirikishwaji wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Wizara inapaswa kuandaa agenda ya kitaifa na mipango mahususi kuhusu kujenga uzalendo kwa Watanzania katika kupenda sanaa zao za ndani. Katika kusaidia kuwezeshwa kurudisha uzalendo wa hadhira ya muziki ya ndani kwenye muziki wao kuna haja ya mipango iliyofanyika miaka ya 1960-1970 katika kuiboresha sanaa ya Kitanzania irejeshwe upya na kwa umakini na kwa wakati wa sasa. Kwa hivi sasa, yabidi kurejeshwa kwa hatua hizo huku zikimakinikia kwa kina miktadha ya kimaendeleo, kiteknolojia, na utandawazi ulioichukua jamii ya Kitanzania. Kwa kufanya hivyo, hadhira ya muziki wa kizazi kipya itaongeza upenzi kwa muziki wao wa ndani. Hivyo, kukuza soko la ndani na ukuzaji wa utamaduni na utalii unaoweza kuibuka kupitia tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili.

**Kumakinikia Mitindo ya Sanaa za Kitanzania katika Utengenezaji wa Muziki**

Fauka ya hayo, makala imeona kuwa kuna haja ya kumakinikia ubunifu katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Wasanii na waandaaji wa kazi za muziki wanahitajika kuongeza ubunifu kuanzia kwenye kuandaa kazi, hadi inapomfikia msikilizaji au/na mtazamaji wa kazi husika. Tumeona kazi zinakuwa na mahadhi ya Kinigeria/kigeni kutokana na suala la ubunifu kutotiliwa maanani wakati wa uundaji wa awali wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Jambo hili, awali, lilionekana dhahiri kupitia mahojiano tuliyoyafanya kupitia wasanii na watalaamu wa eneo la muziki. Pili, lilionekana kwa mdhihiriko mpana kupitia mahojiano baina ya mtangazaji Millard Ayo na Siraju Hamisi (Laizer) - Mtayarishaji mkuu wa muziki kutoka studio za Wasafi Classic. Makala ilibaini kuwa, hali hii imekuwa ikisababisha muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kuanza kuchukua athari kubwa ya Kinigeria kuanzia kwenye mashairi na matamshi ya kuimbia nyimbo hizo, hususani wanapotaka kutumia maneno ya Kiingereza katika nyimbo zao. Athari hizo ndizo huja kuamua muonekano wa video nzima ya wimbo wa kizazi kipya wa Kiswahili.

Hivyo basi, ili kuiondoa changamoto hiyo, inapendekezwa kuwe na kauli moja ya watayarishaji wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Kauli ya kumakinikia mitindo ya sanaa za Kitanzania katika utengenezaji wa ala, midundo na ushauri wa namna muundo wa mashairi katika nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili unatakiwa uwe. Ni imani yetu kuwa, mabadiliko makubwa ya kitasnia yatakuwepo kupitia watayarishaji wa muziki, hususani katika kujenga namna bora ya sanaa ya muziki wa kizazi kipya. Ubunifu huu ukiongezwa, na vyombo vya habari vikiupa nafasi muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania unaweza kuvuta mashabiki wengi katika muziki wao. Kuvutwa huku kwa mashabiki kutatokana na kuona kuwa muziki wao umewakilisha mambo yanayoigusa jamii yao kwa kiasi kikubwa. Nguvu kubwa iwekezwe kwa wayatarishaji wa muziki wa kizazi kipya ili wawe kiini cha utengenezaji wa muziki wanaoufanya. Hivi sasa, mkazo mkubwa uko kwa msanii wa muziki wa kizazi kipya ambaye ndiye huamua nini kifanyike. Maamuzi hayo ya wasanii wa kizazi kipya, aghalabu, huwasukuma watayarishaji wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kutengeneza muziki kuendana na matakwa ya wasanii hao. Watayarishaji wa muziki hufanya hivyo kutokana na wasanii kuwa kiini cha hatua nzima za utengenezaji muziki. Baadhi ya wasanii wa muziki wa kizazi kipya ndio wamiliki wa studio za kurekodia muziki na video. Vilevile, wasanii hao hulipa gharama za hatua zote za utayarishaji wa muziki na video. Hivyo, msanii

anapoleta wazo la wimbo, pia huamua na ala, mdundo na mashairi anayoyataka. Jambo hilo huenda hadi kuathiri utayarishaji wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya kwa kuwa zenyewe nazo hufuata mtiririko mzima wa mashairi.

Katika kuzidi kulifanikisha suala la kutengenezwa kwa muziki wenye alama ya U-Tanzania, tunapendekeza kuwe na vikao vya mara kwa mara baina ya Wizara inayohusika na ukuzaji na uendelezaji wa sanaa nchini Tanzania, pamoja na watayarishaji wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Kupitia vikao vya kujadili muelekeo wa muziki wa kizazi kipya nchini Tanzania, vinaweza kusaidia kutengeneza dira ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Katika kutoa mapendekezo ya kutengeneza dira ya tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili na sanaa nchini Tanzania, tunapendekeza kuwe na mikakati ya dharura ya kupunguza hali iliyopo; pia, kuwe na mikakati ya muda mrefu na endelevu.

Kwa miaka mingi, watayarishaji wa kizazi kipya wamekuwa hawajumuishwi katika kutoa mapendekezo ya ukuzaji na uendelezaji wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Kinachosahaulika ni kuwa chanzo na hatima ya ukamilifu wa muziki wowote huanzia studio. Hivyo basi, endapo watayarishaji watasikilizwa ipasavyo, huenda wakatoa njia nzuri ya kuusaidia muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kutoa taswira ya U-Tanzania wake. Ni imani yetu kwamba, kufanyika kwa jambo hili kutaweza kuhuisha na kuiboresha kwa teknolojia za kisasa za kurekodi mitindo ya ngoma na midundo ya kijamii kama vile "tokomile", "vanga", "mdundiko", "lizombe", na mengineyo. Mitindo na ngoma hizo, hivi sasa, inaonekana kupotea kutokana na dhana kubwa ya utandawazi ambayo imewapatia upofu wa kisaikolojia wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili, pamoja na hadhira yake iliyopo nchini Tanzania. Hamasa kwa watayarishaji wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kuongeza mikong'osio, ala, na midundo ya jamii zinazopatikana nchini Tanzania itasaidia kwa wepesi zaidi kuondokana na unakili wa motifu zinazochotwa kutoka muziki wa Kinigeria.

Vilevile, msisitizo mkubwa unatakiwa kuwekwa kwa watayarishaji na waongozaji wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Watengenezaji wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wanatakiwa wawe na maamuzi makubwa katika kutayarisha video zenye kubeba utamaduni wa Kitanzania. Imethibitika kuwa utayarishaji wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nao umekuwa ukiamuliwa na wasanii wenyewe. Wasanii wamekuwa wakileta mawazo na maamuzi ya mwisho ya namna video ya nyimbo zao ziwe. Watayarishaji na waongozaji wa video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili wamekuwa wakishindwa kutoa ushauri kwa sababu kubwa ya kwamba wasanii ndio wadhamini wa video hizo. Hivyo basi, wamekuwa wakishindwa kwenda kinyume na maamuzi yao. Kwa hali hiyo, tunapendekeza kuwa kuwepo na mgawanyo wa majukumu ya kibunifu. Wakati wa kutayarisha video ya wimbo wa muziki wa kizazi kipya, wasanii wawape nafasi watayarishaji kusana video itakayogusa utamaduni wa Kitanzania. Hili litaondoa ile dhana ya wasanii wa muziki kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kuwashauri watayarishaji wa muziki wa kizazi kipya wawatayarishie video kama msanii fulani wa Kinigeria inayotamba sokoni.

**Kuharakisha Upatikanaji wa Vazi la Taifa**

Wabunifu wa mavazi wa nchini Tanzania wanahitajika kupewa kipaumbele wakati wa ubunifu wa mavazi na maleba yanayotumika katika video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Katika utayarishaji wa mavazi, wabunifu nao wamekuwa wakisukumwa na wasanii wa muziki wa kizazi kipya ambao ni wadhamini na, wakati mwingine, wamiliki wa studio zinazotengeneza video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya. Wabunifu wa mavazi wakipewa nafasi ya kutumia ubunifu wao kusanifu na kushona nguo zitakazoakisi utamaduni wa Kitanzania, watasaidia kubadilisha taswira ya mavazi ya Kinigeria yaliyopo katika video za nyimbo hizo au/na katika maisha ya kawaida ya Kitanzania.

Vilevile, jambo hili litafanikiwa kwa urahisi ikiwa mchakato wa vazi la taifa utahuishwa na kukamilishwa. Zaidi ya miaka ishirini sasa mchakato wa kupata vazi la taifa umeishia njiani[2]. Hivyo, inawawia vigumu wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, pamoja na wabunifu wa mavazi, kujua wapi waanzie katika kutengeneza mavazi yatakayoakisi taifa lao. Kusuasua kwa kutopatikana kwa vazi la taifa kumekuwa kukiwasukuma wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania wawashawishi wabunifu wa mavazi kubuni mavazi yanayoakisi mavazi yenye nasaba ya Kinigeria. Katika kukuza ubunifu wa mavazi yanayoakisi nchi ya Tanzania, imeonekana kuna haja ya Wizara ya Sanaa, Utamaduni, na Michezo pamoja na vyombo vyake vinavyohusika na ukuzaji wa sanaa nchini Tanzania iandae tafiti, warsha, na semina zitakazowahusisha wabunifu wa mavazi wa Kitanzania ili kuwaongezea uwezo wa fani yao na kutengeneza dira ya mavazi kwa nchi ya Tanzania.

**Uundwaji wa Vipindi vya Uchambuzi wa Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya**

Kuna haja ya kuundwa kwa vipindi vya uchambuzi wa muziki na video za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Kwa kitambo kirefu sasa, kumekosekana vipindi vya redio na televisheni vinavyochambua maudhui na fani ya muziki wa kizazi kipya katika mashairi, ala na video. Mwanzoni, kulikuwa na vipindi vya uchambuzi wa nyimbo za muziki wa kizazi kipya katika televisheni ya EATV katika kipindi cha "Planet Bongo" chini ya mtangazaji Salama Jabir. Lakini vipindi vya aina hii vilipungua uzito na kutoweka kabisa kuanzia mwaka 2010. Vipindi hivi vilikuwa vinajitahidi kuweka dira ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Kupotea kwake kumetoa fursa ya msanii wa kizazi kipya kuweza kuunda muziki wake kulingana na hisia na kiu ya msanii pekee.

Kwa hali hiyo, uwekwe msisitizo wa kurudishwa kwa vipindi vya uchambuzi ambavyo vitakuwa na wachambuzi wa muziki wa kizazi kipya watakaokuwa na uwezo wa kufanya uchambuzi wa kina na kufanya ukosoaji makini, hususani kwa wasanii watakaotoa nyimbo na video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili zenye kunakili maudhui, mada, na matamshi ya kigeni. Kufanyika kwa jambo hili kutasaidia kupunguza 'ugeni' katika muziki wenye kuwakilisha U-Tanzania. Upatikanaji wa wachambuzi wa vipindi vya uchambuzi wa muziki unaweza kufanyika kupitia wataalamu kutoka vyuo vikuu na vyuo vingine vinavyohusisha masomo ya sanaa, lugha ya Kiswahili, na utamaduni.

[2] Mchakato wa upatikanaji wa Vazi la Taifa ulianza mwaka 2003/2004 na kufufuliwa tena mwaka 2011. Kisha mchakato wake ukakwama hadi mwaka 2018. Kabla ya kufufuliwa tena mwaka 2022/2023. Hatua zake bado zinaendelea hadi hivi sasa.

Wengine wanaweza kupatikana kutoka miongoni mwa wasanii nguli, pamoja na watangazaji wenye tajriba kubwa ya kufanya kazi katika redio na televisheni kwa miaka mingi, na wenye nia njema ya kuleta mabadiliko chanya yanayohitajika.

**Wasanii Kushawishiwa Kutumia Mandhari ya Kitanzania katika Video**

Tunapendekeza serikali iwe na ushawishi mkubwa kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kuweza kutumia mandhari ya ndani katika kutayarishia video zao. Kufanikiwa kwa jambo hili kunatakiwa kwenda sambamba na kupunguzwa kwa gharama za kulipia vivutio vya kitalii pamoja na majengo ya serikali yatakayohitajika kutumika katika utayarishaji wa video. Vilevile, kupunguzwa kwa urasimu wa kupata vibali vya kurekodi video katika maeneo hayo kutasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kutokwenda nje ya Tanzania kutayarishia video zao. Kwa kufanya hivyo, wasanii wa muziki wa kizazi kipya, kupitia video za nyimbo zao, watazidi kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania kama vile Mlima Kilimanjaro, fukwe za visiwa vya Unguja, Pemba na Mafia, majengo ya kale ya Bagamoyo na Tanga, hifadhi za Serengeti na Ngorongoro pamoja na maeneo mengine. Urahisi wa ufanikishaji wa jambo hili utategemea mawasiliano ya kikaribu kati ya Wizara za Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Habari, Teknolojia na Mawasiliano, Wizara ya Utalii na Maliasili na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.

**Kuanzishwa kwa Matamasha na Tuzo za Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania**

Tunapendekeza kuanzishwa kwa matamasha ya kuenzi muziki wa asili wa Kitanzania yatakayoenda sambamba na matamasha ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili. Kuwapo kwa matamasha haya kutasaidia kuhifadhi utamaduni wa mila za Kitanzania. Pia, yatasisimua ubunifu kwa wasanii wa kizazi kipya wa Kiswahili kuweza kutumia motifu za muziki wa asili wa Kitanzania katika kuunda muziki wao. Zaidi, kutafanikisha utayarishaji wa video wa nchi ya Tanzania kuwa na aina yake ya muziki utakaoitambulisha nchi nje ya mipaka. Aidha, kupitia matamasha haya, wasanii wanaochipukia watapata mahala pa kuanzia kuchukua vionjo vitakavyonyanyua ubunifu wao kuelekea kuwa wasanii wakubwa. Hadi sasa hakuna matamasha makubwa yenye dira ya kunyanyua utamaduni wa Kitanzania kupitia tasnia ya muziki. Tamasha kubwa la muziki wa Kitanzania la Kilimanjaro (*Kilimanjaro Music Awards*) lilifanyika kwa mara ya mwisho mwaka 2013.

Vilevile, katika kwenda sambamba na matamasha ya muziki wa kiasili na muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, suala la tuzo kwa wasanii linatakiwa kupewa kipaumbele pia. Ni muhimu kuanzishwa tuzo za muziki zitakazotambua nyimbo na video za nyimbo za muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili zinazoutambulisha utamaduni wa Kitanzania. Litakuwa jambo jema tuzo hizi zikijumuisha zawadi ya fedha au vyombo vya kupigia au/na kurekodia muziki. Zawadi za washindi zinaweza kutolewa na mashirika ya kiserikali, mashirika binafsi au/na asasi za kiserikali. Yote ikiwa ni katika kuzidi kuwavuta wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili kurudi katika uasili wao. Tuzo hizo zinaweza kujumuisha wimbo bora wenye ala na mdundo unaoakisi jamii ya Kitanzania, matumizi ya vazi bora la kiasili la Kitanzania katika video ya wimbo wa kizazi kipya wa Kiswahili au/na mitindo bora ya uchezaji wa kiasili iliyojitokeza katika video. Ni imani yetu kuwa tuzo zitasaidia kuhamasisha wasanii wengi wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kuandaa nyimbo na video za nyimbo zenye mahadhi ya Kitanzania. Kwa hiyo, wasanii watakapofanikiwa kuchukua vionjo vya Kitanzania katika kazi zao za kisanaa watapunguza uigaji na

unakili wa moja kwa moja wa motifu za Kinigeria katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania.

**Mitalaa ya Biashara, Lugha ya Kiswahili, na Utamaduni wa Kitanzania**

Tunapendekeza kuwepo na uandaaji thabiti wa utengenezaji wa mitalaa yenye kuhusisha biashara ya muziki wa kizazi kipya, lugha ya Kiswahili, sanaa, na utamaduni wa Kitanzania. Vilevile, tunapendekeza kuwe na ukaribu wa kimahusiano baina ya taaluma ya Sanaa za Fani ya Lugha na Fasihi ya Kiswahili, Sanaa za Maonesho, Filamu na Video za Kiswahili, Utalii na Utamaduni wa Kitanzania. Kupitia utafiti, ilibainika kuwa idara za kitaaluma katika vyuo vikuu nchini Tanzania ziko mbali katika mahusiano ya kitaaluma. Idara za Lugha na Fasihi zimekuwa zikijitegemea zenyewe bila ya kuhusisha Idara za Sanaa za Maonesho na Filamu, hivyo kupunguza nguvu ya mahusiano ya kitaaluma na ukuaji wake. Kutokana na maendeleo makubwa ya kisayansi na kiteknolojia, kuna haja ya kuwa na mahusiano ya kitaaluma baina ya idara hizi ili kuweza kuzidisha soko la ajira kwa wanafunzi wanaotoka katika vyuo vikuu na asasi za kisanaa, hususani wanaosoma masomo ya kifasihi. Masomo kama vile Filamu ya Kiswahili, Uandishi wa Filamu za Kiswahili, Uwekaji Tafsiri na Sauti katika Filamu na Uteuaji wa Kazi Mfano za Kifasihi kuwa Filamu ni muhimu yakipatiwa nafasi katika Idara za Lugha na Fasihi ili kuweza kuongeza wigo wa kiajira kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya Isimu, Tafsiri na Fasihi katika vyuo na taasisi za kielimu.

**Kuwe na Muumano Mzuri kati ya Biashara, Utamaduni na Matumizi ya Teknolojia**

Jambo la mwisho ambalo tunalipendekeza ni wasanii wa muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania kutambua muumano wa suala la biashara ya muziki, utamaduni wao, pamoja na maendeleo ya kiteknolojia yanayoibuka kila uchao. Wasanii wanatakiwa kutambua kuwa, licha ya kukimbilia katika biashara, hawatakiwi kuwa mbali na utamaduni wao ambao wanaweza kuufanya biashara. Makala imebaini kuwa, wasanii wanatakiwa kuitumia vema teknolojia bila kuchotwa na nguvu ya tamaduni za kigeni. Vilevile, vyombo vya usimamizi viweke njia nzuri ya kuhakiki muziki huu kutegemeana na ukubwa wa kiteknolojia uliopo hivi sasa, pamoja na njia zake za kimawasiliano ambazo ni rahisi kuufanya muziki kuwafikia watu. Mazingira yatengenezwe kuanzia hatua za mwanzo ili kazi zinazotoka ziwe zina mwelekeo sahihi wa kimaadili; badala ya kusubiri mwisho kutoa hukumu. Katika kuufanya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili uweze kuongeza kani za ukuaji, kuna haja ya serikali kutengeneza mfumo mzuri utakaowezesha makampuni makubwa katika sekta binafsi kufanya uwekezaji katika tasnia ya muziki huu. Makampuni hayo yahusishe asasi za kifedha ambazo zinaweza kuwekeza moja kwa moja katika tasnia au/na kuwezesha mitaji ya kusaidia uandaaji wa nyimbo na video za nyimbo zitakazogusa tamaduni za Kitanzania kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia ya kidunia. Makampuni mengine yanayoweza kushauriwa kuwekeza katika tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania, ni kama vile makampuni ya simu, makampuni ya vinywaji (vilevi na vinywaji baridi), makampuni ya ubashiri katika michezo, makampuni ya vifaa vya kielektroniki na mengineyo.

**Hitimisho**

Kupitia tathimini iliyofanyika na makala hii, ni imani yetu kuwa mapendekezo haya yakitiliwa mkazo, yanaweza kusaidia kuondoa tishio la utamaduni wa Kinigeria unaozidi kuchukua kazi katika muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania na maisha ya wa-Tanzania kwa jumla. Zaidi,

yatavisaidia vyombo vilivyopewa dhima ya kukuza na kuendeleza sanaa na lugha nchini Tanzania kuandaa programu zao zitakazowasaidia wasanii wa muziki wa kizazi kipya, watayarishaji wa muziki, watayarishaji wa video, wabunifu wa mavazi pamoja na wabunifu wengine kuiona fursa ya kuitumia amali iliyopo katika utamaduni wa Kitanzania kujitangaza na kujiletea kipato. Vilevile, kuwapo kwa misingi imara ya uhakiki na utoaji elimu katika hatua za mwanzoni mwa ubunifu kutasaidia kuondoa ulazima wa ufungiaji wa nyimbo na kusababisha hasara katika biashara ya muziki. Ufanikiwaji wa jambo hili utategemea ushirikishwaji wa karibu baina ya wadau wa sanaa, watayarishaji, waimbaji, wadau wa utamaduni, na wananchi kwa jumla katika mikakati ya ukuzaji wa sanaa nchini Tanzania.

Kwa hiyo, kwa pamoja, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), na Vyuo Vikuu vinavyotoa fani ya sanaa na lugha ya Kiswahili wana jukumu kubwa la kuandaa programu na mikakati yenye kutoa dira ya tasnia ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili nchini Tanzania. Tunaamini kuwa kufanyika kwa mambo tuliyoyapendekeza kutasaidia kwa kiwango kikubwa katika kuleta na kusimamia uwepo wa sanaa ya muziki wa kizazi kipya wa Kiswahili yenye kubeba utambulisho wa Kitanzania.

## Marejeleo

Devereux, A. (2010). *A Triangular Approach to Science Filmmaking* (M.F.A Thesis, Unpublished). Montana State University, Montana.

Haynes, J., & Onookome, O. (eds). (2000). *Nigerian Video Films*. Ohio University Press and Swallow Press.

Jengo, E., Mbughuni, L., A & Kandoro, S. A. (Wahariri). (1982). *Falsafa ya Sanaa Tanzania*. Baraza la Sanaa la Taifa.

Kasiga, G. A. (2022). "Tathimini ya U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya wa Kiswahili nchini Tanzania". Tasnifu ya Uzamivu, (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kasiga, G. A. (2021). "Athari za U-Nigeria katika Video za Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya Nchini Tanzania", *Ruaha Journal of Arts and Social Sciences (RUJASS)*, 7 (1): pp. 118-135.

Kasiga, G. A. (2019). *Mwanzo na Mdhihiriko wa U-Nigeria katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania.* Ponera, A.S, & Badru, Z. A. (Wahariri). *Koja la Taaluma za Insia*: *Kwa Heshima ya Profesa Joshua Madumulla*, Karljamer Publisher Limited, 663 – 680.

Kasiga, G. A. (2018). "U-Nigeria: Athari zake katika Filamu za Kiswahili nchini Tanzania". *Mulika*, 37, pp. 72-84.

Kasiga, G. A. (2013). "U-Nigeria katika Filamu za Ki-Tanzania: Chanzo chake, Sababu za Kutumiwa na Athari zake kwa Wa-Tanzania". Tasnifu ya Umahiri, (Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mrikaria, S. E. (2007). "Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya", *Swahili Forum* 14: pp. 197- 206.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEPL.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Moccony Printing Press.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Mwanafunzi na Mwalimu wa Fasihi Simulizi na Andishi.* MVP.